JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA MIPANGO KABAMBE (MASTER PLANS) ILIYOIDHINISHWA KWENYE MAMLAKA ZA UPANGAJI



Tamko la Katibu Mkuu

Serikali ya Jamhuri ya muungano ya Tanzania inalo jukumu la kutekeleza matakwa ya wananchi wake yanayoainishwa kwa mujibu wa katiba ya nchi. Ardhi ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla na hivyo inahitaji kuandaliwa mipango ya jumla ya uendelezaji.

Mipango ya jumla ambayo inahusisha Mipango Kabambe, Mipango ya matumizi ya ardhi na Mipango ya muda wa kati inaandaliwa kwa ajili ya kuongoza ukuaji wa Miji na vijiji. Mipango hii huandaliwa kwa mujibu wa sheria ya Mipango miji Namba 8 ya mwaka 2007 na sheria ya matumizi ya Ardhi Namba 6 ya mwaka 2007. Kwa mujibu wa sheria hizo mamlaka za upangaji ni Majiji, Manispaa, Miji, Miji Midogo na Vijiji.

Ofisi ya Rais -TAMISEMI ndiyo yenye jukumu la kusimamia utekelezaji wa Mipango Kabambe kwa ajili ya uendelezaji wa Miji na Vijiji. Zimejitokeza changamoto za utekelezaji wa Mipango Kabambe ya Uendelezaji kwenye Mamlaka za Upangaji. Changamoto hizi zinatokana na kutokuwepo kwa Mwongozo wa utekelezaji wa Mipango Kabambe kwenye Miji na Vijiji Nchini ambao umechangia uendelezaji holela wa ardhi.

Kufuatia changamoto hizo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeona umuhimu wa kutoa Mwongozo ambao unaweka utaratibu wa kusimamia utekelezaji wa Mipango Kabambe inapokuwa imeidhinishwa. Aidha, Serikali kupitia Ofisi ya Rais-TAMISEMI ina imani kwamba Mwongozo huu utatumika na kusimamiwa ipasavyo na Mamlaka za Serikali za Upangaji pamoja na wadau wengine walioainishwa katika Mwongozo huu.

Utekelezaji wa Mwongozo utaiwezesha Miji na Vijiji kuendelezwa kwa mpangilio stahiki kama inavyochanganuliwa kwenye Mipango hiyo Kabambe. Watekelezaji wa Mipango hiyo ni wananchi, ofisi za Mitaa, Kata, Wataalam wa Halmashauri wa sekta zote, Wanasiasa na viongozi wa sekta na Taasisi mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali pamoja na wadau wengine wa ndani na nje ya nchi.

Mwongozo huu ni nyenzo muhimu itakayosaidia kusimamia utekelezaji wa Mipango Kabambe kwenye Mamlaka za Upangaji nchini. Hivyo, naelekeza Mamlaka zote za Upangaji kutekeleza Mwongozo huu ipasavyo ili kuleta tija katika uendelezaji wa Ardhi Nchini.

Prof. Riziki S. Shemdoe
KATIBU MKUU
OFISI YA RAIS-TAMISEMI

Juni, 2022

1. Utangulizi

Ofisi ya Rais TAMISEMI, ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa sera zote kutoka Wizara za kisekta. Watalam wa Sekta zote wanapatikana kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo ni Mamlaka za Upangaji. Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinaundwa na Watendaji yaani Wataalam wakiongozwa na Wakurugenzi wa Halmashauri na Mabaraza ya Madiwani yakiongozwa na Mameya na Wenyeviti wa Halmashauri.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatekeleza matakwa ya wananchi wake yaliyoainishwa kikatiba. Majukumu haya yameainishwa kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala, *malengo endelevu ya maendeleo 2030 lengo Na.11 linalohusu Miji endelevu.* Uandaaji na utekelezaji wa Mipango Kabambe unajumuisha sekta zote kwa sababu ya uhitaji wa huduma zote za kijamii, miundo mbinu na kukuza uchumi.

Ardhi ni rasilimali kuu inayohitaji nyenzo za aina mbalimbali za kuiendeleza ili kuwaletea wananchi maendeleo. Hivyo inahitaji kuandaliwa Mipango endelevu kwa ajili ya matumizi ya sasa na vizazi vijavyo. Mipango hiyo itaongoza ukuaji wa Miji na Vijiji. Aidha, uandaaji wa Mipango Kabambe umekuwa ukifanywa na Mamlaka za Upangaji kwa usaidizi wa wataalam mbalimbali ndani ya Halmashauri husika; na baadae kupata idhini kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wanaoratibu uidhinishwaji kisheria.

Katika hatua za maandalizi Mamlaka za Upangaji kupitia Kamati zenye jukumu la kusimamia maendeleo ya ardhi na kwa kushirikisha Wananchi ambako Mpango unaandaliwa huhitajika kutoa maoni juu ya matarajio waliyonayo kuhusu kupata majibu ya masuala muhimu yanayohusu fursa na vikwazo katika maendelo.

Hata hivyo, Utekelezaji wa Mipango Kabambe umekuwa ukisuasua kutokana na changamoto ya kutokuandaliwa kwa Mipango ya kina; Mipango ya kina kutokufuata takwa la Mpango Kabambe; Uvamizi wa maeneo ya wazi na maeneo hatarishi; kukosekana kwa miiundombinu ya kuchakata takwimu za Kijiografia; upungufu wa Wataalam na ukosefu wa Rasilimali fedha. Hivyo Mwongozo huu utawezesha Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Sekretariet za Mikoa kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Mipango Kabambe kwenye Mamlaka za Upangaji.

1.1. Umuhimu wa Mwongozo

Mwongozo huu wa utekelezaji wa Mipango Kabambe (Master Plans) kwa sasa umepata umuhimu kutokana na changamoto kwamba; Miji iliyotayarishiwa Mipango Kabambe bado inaendelezwa pasipo kufuata Mipango iliyoidhinishwa. Aidha, kutokuwepo kwa Mwongozo kwa Mamlaka za Upangaji wa kuongoza

utekelezaji wa mipango hiyo baada ya kuidhinishwa hautekelezwi ipasavyo kutokana na kukoseka kwa bajeti ya uendelezaji wa Mipango hiyo; kutokuwepo kwa miiundombinu ya kuchakata takwimu za Kijiografia ili kuwa na kanzi data za kisekta katika Mji husika; Wadau wa Sekta zingine hawajajulishwa na kuratibiwa kwenye suala la utekelezaji wa Mpango Kabambe kwa kuwa shughuli zao ziko ndani ya Mpango kama walivyopendekeza kipindi cha Kuandaa Mpango Kabambe waliposhirikishwa.

1.2. Lengo la Mwongozo

Mwongozo huu unalenga kuweka utaratibu wa kusimamia utekelezaji wa Mipango Kabambe iliyoidhinishwa mara inapokuwa imekabidhiwa kwa Mamlaka za upangaji ili kuendelea na utekelezaji. Halmashauri itahusika na kazi ya kuratibu wadau mbalimbali kwa kadiri walivyoainishwa kwenye Mpango Kabambe. Kila sekta iatashiriki hatua hii muhimu ya utekelezaji kwa uratibu madhubuti wa Mamlaka za Upangaji.

2.0 Walengwa wa Mwongozo

Mwongozo huu umetolewa kwa ajili ya Wadau wote wa maendeleo kwenye Mamlaka za Upangaji wanaoshiriki katika utekelezaji wa Mipango Kabambe nchini:

2.1 Majukumu ya Wadau

2.1.1 Katibu Tawala wa Mkoa

a) Atakuwa Msimamizi Mkuu wa Utekelezaji wa Mipango Kabambe yote iliyoidhinishwa kwenye Halmashauri za Mkoa wake.

b) Atateua Timu ya Wataalam ya usimamizi wa utekelezaji yenye wajumbe wasiopungua 10 (kumi) kutoka miongoni mwa wajumbe wa CMT, Wadau kutoka Sekta Binafsi, Makampuni na Taasisi za Kiserikali na zisizo za kiserikali. Katika kutekeleza jukumu hili, atashirikiana na Mkurugenzi wa Halmashauri husika kufanya uteuzi wa Wajumbe husika.

Majukumu ya Timu ya Wataalam itakuwa ni:-

i. Kupokea, kushauri na kuidhinisha Mipango ya kina ya uendelezaji kutoka kwa Wadau mbalimbali.

ii. Kupokea na kupitia Taarifa za Mfumo wa Kijiografia (GIS) ili kubaina hali halisi na mwenendo wa utekelezaji wa Mpango Kabambe.

2.1.2 Mkurugenzi wa Jiji/ Manispaa/Miji/Wilaya

a) Kupokea taarifa ya utekelezaji kutoka katika timu ya Wataalam ya usimamizi wa utekelezaji wa Mpango Kabambe.

b) Atakuwa msimamizi Mkuu wa kutekeleza Mpango Kabambe.

c) Kutoa taarifa ya utekelezaji kwenye Baraza la Halmashauri mara Nne kwa mwaka.
d) Atashirikiana na Katibu Tawala wa Mkoa kuteua timu ya usimamizi wa Mpango Kabambe.
e) Kuwasilisha kwa Katibu Tawala wa Mkoa taarifa ya utekelezaji wa Mpango Kabambe.
f) Mkurugrenzi ataratibu vikao na wadau katika utafutaji wa rasilimali zinazohitajika kwenye utekelezaji.
g) Kuandaa Sheria ndogo ili kuboresha usimamizi wa utekelezaji wa Mpango Kabambe.

2.1.2 Idara ya Miundombinu, Uendelezaji wa Vijiji na Miji

a) Kufanya mgawanyo (*zoning*) wa maeneo uwandani kwa kuweka alama za maeneo husika.
b) Kutambua Wananchi wenye Maeneo ndani ya Mpango.
c) Kuratibu uandaaji wa Mipango ya Kina ya utekelezaji wa Mpango Kabambe.
d) Kutoa elimu kwa wananchi wenye maeneo yaliyotambuliwa kwa mujibu wa Mpango Kabambe.
e) Kuandaa Kanzi data za kisekta ili wahusika wapatiwe kurahisha utekelezaji na ufuatiliaji kazi uwandani.

2.1. 3. Idara za Halmashauri

Idara na Vitengo zinazounda Halmashauri zitakuwa na majukumu yafuatayo: -

a) Kutekeleza maeneo ya Sekta yake ya Idara/Kitengo yaliyoainishwa kwenye Mpango Kabambe.
b) Kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango kwa sekta yake.
c) Watatakiwa kutoa taarifa ya kinachotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka husika na mahitaji, kwenye vikao vya menejimenti wakati wa kuandaa bajeti.

2.5.1 Kamati ya Maendeleo ya Kata

Kamati ya Maendeleo ya Kata itakuwa na wajibu wa kusimamia yafuatayo: -

a) Kuhakikisha kuwa, Maendelezo yote yanayofanywa kwenye Kata yanafuata Mpango Kabambe.

a) Kutoa taarifa kwa Mkurugenzi kuhusu maendelezo yanayofanyika kwenye maeneo yao.

b) Kila mwaka wafanye tathmini ya kuendeleza maeneo ndani ya Kata na kupata taswira za hali ya uendelezaji.

2.6. Halmashauri ya Mtaa/Kijiji

Halmashauri ya Mtaa/Kijiji itatakiwa kusimamia yafuatayo:

a) Kuhakikisha kuwa, Maendelezo yote kwenye Kijiji/Mtaa yanafuata Mpango Kabambe.

b) Kutoa taarifa kwenye Kamati ya maendeleo ya Kata kuhusu maendelezo yanayofanyika kwenye maeneo yao.

2.4 Wadau wa Sekta za Umma na Binafsi

Wadau wa Sekta za Umma na binafsi watawajibika kufanya yafuatayo: -

a) Kushiriki kwenye vikao vitakavyoitishwa na Mkurugenzi kuhusiana na utekelezaji wa Mpango Kabambe.
b) Kuandaa Mpango kazi na kutenga Bajeti ya kutekeleza maeneo yaliyoainishwa kwenye Mpango Kabambe.
c) Kutoa elimu kwa Umma kuhusu utekelezaji wa Mpango Kabambe.

3.0 Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Mwongozo

Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo huu itafanyika kila kipindi cha miezi sita tangu kuanza kutumika kwa Mwongozo huu ili kubaini mafanikio katika kufikia malengo ya Mwongozo. Tathmini itaonesha changamoto zilizojitokeza katika utekekelezaji na hivyo kutoa mapendekezo yatakayofanyika ili kuboresha utekelezaji wa Mpango Kabambe kama inavyoelekezwa na Mwongozo huu.

4.0 Mfumo wa Utoaji Taarfia

Mkurugenzi katika Halmashauri ya Mji husika atawasilisha kwa Katibu Tawala wa Mkoa husika taarifa ya utekelezaji wa Mpango Kabambe na Taarifa hiyo itawasilishwa Ofisi ya Rais TAMISEMI kila baada ya miezi mitatu. Taarifa hizo zitasaidia kubainisha kiwango cha utekelezaji na uzingatiaji wa Mpango Kabambe na changamoto zilizojitokeza kipindi cha utekelezaji wake ili kupanga namna ya kuondosha changamoto hizo.

5.0 Mapitio ya Mwongozo

Mwongozo huu utafanyiwa mapitio kulingana na mahitaji kadiri yatavyojitokeza katika kipindi cha utekelezaji wake.

6.0 Hitimisho

Mwongozo huu umeandaliwa kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Mipango Kabambe iliyoidhinishwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hivyo Wakurugenzi wa Mamlaka za Upangaji, watatakiwa kuutumia Mwongozo huu na kutoa taarifa za utekelezaji wake Ofisi ya Rais – TAMISEMI.